TANGAZO LA SERIKALI Na. 812 la tarehe 10/11/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA NG'HAYA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Ng'haya ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Eneo la Upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa eneo

3. Mipango ya jumla na ya kina kwenye eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

JEDWALI

*(Iimetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV670 yenye majira-nukta 565353MS, 9710431KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS170$^{0}$03’40”MG kwa umbali wa kilomita 2.691 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV641 yenye majira-nukta 565814MS, 9707780KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS180$^{0}$09’00”KS kwa umbali wa kilomita 1.405 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV236 yenye majira-nukta 565819MS, 9706374KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS55$^{0}$30’50”MG kwa umbali wa kilomita 2.824 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV241 yenye majira-nukta 564173MS, 9704076KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG99$^{0}$11’10”MG kwa umbali wa kilomita 3.621 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV233 yenye majira-nukta 560599MS, 9704654KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ117$^{0}$03’20”MG kwa umbali wa kilomita 1.470 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV239 yenye majira-nukta 559290MS, 9705322KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ208$^{0}$56’40”MS kwa umbali wa kilomita 3.297 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV237 yenye majira-nukta 560885MS, 9708207KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ63$^{0}$32’40”MS kwa umbali wa kilomita 4.990 hadi ulipoanzia.

Dodoma,
19 Oktoba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*